**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Januari, 2026**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI**
**YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA**

Anwani ya simu "**MKUU WA SHULE**" SHULE YA SEK- LIUGURU WASICHANA

Simu :**0785984380/ 0628927418** S.L. P 122

Barua pepe: halimamrope18@gmail.com RUANGWA-LINDI

1/12/2025

JINA LA MWANAFUNZI: ……………………………

**………………………………………………………………**

**S.L.P……………………………………………………**

………………………………………………………

**YAH: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YASEKONDARI YA WASICHANA LIUGURU MWAKA 2026</u>**

Kwanza nachukua nafasi hii kukupongeza kwa kufanya vizuri katika mtihani wa darasa la saba mwaka 2025 HONGERA SANA.Pili nafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na masomo ya elimu ya sekondari ya Kidato cha kwanza katika Shule hii mwaka 2026.Shule ina mandhari na mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunzia.

Shule ya Sekondari ya wasichana (Liuguru Girls) ipo katika Halmashsuri ya Wilaya ya Ruangwa, kata ya Narungombe,kijiji cha liuguru mkoa wa Lindi.Shule ya sekondari ya wasichana Liuguru ipo umbali wa kilomita **3** kutoka Ruangwa mjini. Aidha, Shule ipo kilometa moja Mashariki mwa kijiji cha Chunyu, utaona kibao cha shuleya sekondari ya wasichana Liuguru. Ili uweze kufika shuleni kwa urahisi kutokea Ruangwa mjini panda bodaboda na utalipa shilingi 5000/= hadi shuleni.

Muhula wa masomo utaanza tarehe **05 Januari 2026**, unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **03 Januari 20** kabla au ifikapo saa **10:00 Alasiri.**

Endapo utabadilisha shule/kwenda shule binafsi, tafadhali tujulishe ili tuweze kuhamisha taarifa zako kwenye mfumo wa Usajili (PREMS) na kutoa taarifa kwa mamlaka husika ili kujaza nafasi iliyowazi.

Nawatakia maandalizi mema na safari njema ya kuja shuleni

**KARIBU SANA**

**HALIMA H. MROPE**

**MKUU WA SHULE**

**SIMU;0785984380**

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

## 1.0 SARE YA SHULE

(a) Mwanafunzi aje na sare zenye muonekano ufuataao:

- Sketi 2 za rangi ya **chenza(orange)** kitambaa kizito skert zake ziwe na (belt) mkanda mpana, upana wa belt usizidi sentimeta tano au inchi moja na nusu pia ziwe na urefu usiozidi sentimeta 18 au inchi saba na nusu kutoka kwenye kisigino hadi pindo la skert.Mshono wa skert ni linda box mbele na nyuma na pembeni baada ya linda box yawepo malinda madogo matano.
- Mzazi/mlezi na mwanafunzi tafadhali zingatia vipimo hivyo, mwanafunzi atakayeshona na kuja na sketi kinyume na vipimo, rangi na aina ya kitambaa tulichoelekeza hatapokelewa;
- Shati nyeupe mbili (2) za mikono mifupi tetroni, au nusu kanzu mikono mirefu pamoja na juba kwa wanaovaa hijabu

(b) Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba (visiwe na kisigino kirefu-high heels) jozi mbili (2);

(c) Soksi nyeupe jozi mbili wakati wa masomo na soksi nyeusi jozi mbili kwa ajili ya michezo na wakati wa usiku (Preparat)

(d) Bukta nyeusi kwa ajili ya michezo

(e) Raba nyeupe kwa ajili ya michezo

(f) ~~Truck suit nyekundu isiyobana yenye ufito mweupe pembeni (red white strips) inapatikana shuleni kwa Tsh. 20,000/=~~

~~(g) T-shirt moja (1) rangi ya kijivu yenye kola na nembo ya shule (inapatikana shuleni kwa Tsh.20,000/=)~~

(h) Magauni mawili (Shamba dress) rangi ya Maroon (damu ya mzee).Mshono wa solo yene mikono mirefu na juba kwa wanaovaa hijabu, na mikono mifupi kwa wasiovaa hijabu, liwe gauni lililoshuka hadi chini na lisilobana.,

(i) Sweta moja rangi ya kijivu (Grey)inapatikana shuleni kwa Tsh. ~~12,000/=~~

(j) T-shirt rangi ya zambarau (violet) kwa ajili ya kuvaa siku za michezo yenye kola na nembo ya shule (inapatikana shuleni kwa ~~Tsh. 20,000/=)~~

(k) Mwanafunzi anatakiwa kuwa na kitambulisho cha shule kinachopatikana shuleni kwa gharama ya tsh ~~5000/=~~

(l) Sketi nyeusi mshono kama sare za darasani kama inavyoelekeza sehemu (a) hapo juu

## 1.1 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo:

i. Awe na sanduku (nunua sanduku la bati) linalofunga vizuri;kwa kuhifadhi nguo na vifaa vya vingine
ii. Aje na godoro moja la futi mbili na nusu kwa 6
iii. Shuka mbili za kulalia rangi ya pink isiyo na maua wala urembo wowote
iv. Foronya ya pink isiyo na maua au urembo wowote;
v. Awe na chandarua/net rangi ya pink
vi. Taulo za kike za kutosha
vii. Taulo la kuogea/bafuni rangi yoyote
viii. Kandambili kwa ajili ya kuogea
ix. Viatu vya plastiki (yebo) rangi yoyote vya kushindia
x. ~~Aje na jembe moja na mpini wake~~
~~xi.~~ ~~Aje na soft broom moja~~
~~xii.~~ ~~Aje na Hard broom moja~~
~~xiii.~~ ~~Aje na Mfagio wa kukaushia maji (mopper) moja~~
~~xiv.~~ ~~Aje na ufagio wa kukaushia maji chooni(rubber squizer)~~
~~xv.~~ ~~Fagio la chelewa moja la mti, Pamoja na kwanja~~
~~xvi.~~ ~~Brush ngumu moja ya kusugulia choo yenye mpini mfupi kwa ajili ya kusafishia sinki la choo~~
~~xvii.~~ Aje na Ndoo ndogo mbili (kwa matumizi ya shule na matumizi binafsi)
xviii. Awe na container lenye mfuniko, bakuli, kikombe na kijiko
xix. Daftari (kaunta books) Quire three zisizopungua kumi na moja (11)
xx. Ream mbili ya karatasi A4 (photocopy paper) kwa mwaka
xxi. Mathematical set moja kwa matumizi yake awapo darasani;
xxii. Graph pad moja kwa mwaka
xxiii. Aje na kamusi (dictionary) ya lugha ya kiingereza (English to English)
xxiv. Kama ana bima ya afya aje nayo na kama hana, mzazi au mlezi mkatie kabla ya kuripoti. Aidha, shule inao utaratibu wa kuwakatia Bima ya afya ya NHIF wakiwa shuleni kwa gharama ya **Tsh. 50,400/=** tu(**ni muhimu kila mtoto awe na bima ya afya**)
xxv. Aje na sabuni ya chooni ya maji lita tano (galon moja)
xxvi. Aje na box file moja la kutunzia majaribio yake

**ZINGATIA**

Malipo yote ya shule yafanyike kupitia **AKAUNTI NO.71101100089 LIUGURU SECONDARY SCHOOL, RECCURENT**, benki ya **NMB** na mwanafunzi afike na risiti/hati ya kuweka fedha benki. **Hatutapokea mchango mkononi**.

## 2.0 CHAKULA

Kama zilivyo shule zote za bweni za serikali, shule ya sekondari ya wasichana Liuguru hutoa chakula safi na salama ambacho serikali imeelekeza kitolewe. Endapo unayo miiko ya kutokula baadhi ya vyakula, shule haitatoa huduma ya chakula Maalum (pekee) kwa kila mwanafunzi. Aidha, Pia shule haitoi kibali cha mwanafunzi kujipikia na haturuhusu mwanafunzi kununua aina yoyote ya chakula/kinywaji kutoka nje.

## 3.0 NGUO NYINGINE

- Mwanafunzi aje kitenge doti moja tu, mwanafunzi aje kuripoti akiwa amevaa sare ya shule, shamba dress au track suit (nyekundu). Mwanafunzi hatapokelewa endapo atakuja na nguo za nyumbani;
- Endapo mwanafunzi atabainika kuwa na nguo zisizoruhusiwa akiwa shuleni, atarudishwa nyumbani kurejesha nguo hizo kwa gharama zake.
- Aidha. Masanduku/mabegi makubwa hayaruhusiwi, kwani shule haina nafasi ya kuyatunza**. Mwanafunzi akifika nalo atalazimika kulirudisha nyumbani kwa gharama zake.**

## 4.0 MAELEZO YA ZIADA KWA MZAZI/MLEZI

(a) Shule inafuata mihula inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi Teknolojia (WyEST), hivyo Mzazi/mlezi unaombwa kutoa ushirikiano wako kuhakikisha mtoto wako anaripoti kwa wakati shuleni;

(b) Mawasiliano yoyote kati ya mwanafunzi na mzazi/mlezi yafanyike kupitia simu ya mkuu wa shule;

(c) Maombi ya ruhusa ya mwanafunzi kurejea nyumbani yapitie ofisi ya Mkuu wa shule; Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa sababu za lazima tu mfano Matibabu au Msiba wa Wazazi/Walezi.

(d) Wageni wanao tambulika shuleni ni wale walioandikishwa kwenye faili la mwanafunzi na wanaruhusiwa kumtembelea mwanafunzi mara moja kwa kila mwisho wa mwezi JUMAMOSI itakayoangukia aidha tarehe (27,28,29 30 ,31)

(e) Wakati wa Likizo, mwanafunzi wote watalazimika kurejea nyumbani

## 5.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na teknolojia, yenye dhamana ya elimu chini ya ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo amabayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kufika shuleni:

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima

(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)

(d) Kuwahi kwa kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa

(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako shule hii.

(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule

(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa

(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

(i) Kutunza mali za shule

(j) Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari/Mtaalamu wa Afya;

(k) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni

(l) Mwanafunzi hataruhusiwa kusuka nywele, wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.

(m) Ni marufuku kuvaa kandambili wakati wa chakula katika bwalo

(n) Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi atakayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi

(o) Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu

## 5.1. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA

i. Wizi
ii. Uasherati na usagaji
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo, kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu;
iv. Kutoa lugha chafu na zisizo na utu/maadili kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Ubakaji
vi. Ulevi;
vii. Matumizi ya vilevi na madawa ya kulevya kama vile pombe, bangi, sigara, n.k
viii. Kupigana na mwanafunzi, mwalimu au mtu yeyote yule;
ix. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma;
x. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xi. Kutoa mimba au kusaidia vitendo vya kutoa mimba;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kudharau bendera ya Taifa na Wimbo wa Taifa,Na viongozi wa kitaifa
xiv. Kumiliki, kukutwa na simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kukataa/kudharau adhabu iliyotolewa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua;
xvii. Kutokuhudhuria masomo kwa Zaidi ya siku 90 bila sababu za msingi;
xviii. Kuongea kingereza muda wote awapo shuleni

## 6.0. VIAMBATANISHO MUHIMU VINAVYOPASWA KUKABIDHIWA SHULENI NA MWANAFUNZI PINDI TU ANAPORIPOTI

- Fomu ya kupimwa afya yake (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
- Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule
- Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa wanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

**TAHADHARI;**

Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na matukio ya utapeli (wizi kwa njia ya mtandao) yanayohusisha wanafunzi waliopo shule za bweni. Hivyo, unasisitizwa kuwa;

***Upatapo ujumbe/Taarifa yoyote kuhusu Mwanafunzi/Mtoto wako, Tafadhali usitume chochote kwa Mhusika kabla ya kuwasiliana na Uongozi wa shule ili kupata taarifa sahihi.*** **Kwa mawasiliano yote, Tafadhali wasiliana na wafuatao;**

1. **MKUU WA SHULE** 0785984380/0628927418/0683494937
2. **MAKAMU MKUU WA SHULE** 0627431990/0659242221

***ELIMU KWA MAFANIKIO ENDELEVU***

***HALIMA H. MROPE***

***MKUU WA SHULE***

***0785984380/0628927418***

**FORM NO.1: MEDICAL EXAMINATION**

**PRESIDENT'S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

Liuguru Girls Secondary School

P.O BOX 122

RUANGWA

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**.

Please examine Miss

…............................................................................................................ as her physical and

Mental fitness for admission as a form …………………….. Students at Liuguru Girls' Secondary School in the year ………………

Your sincerely.

HALIMA H. MROPE

HEADMISTRESS

The headmistress,

I have examined Miss as

shown and consider that she is physically and mentally fit/unfit for admission to pursue a full-time secondary school education.

1. Vision with/without glasses. Right ……………………… Left ………………………

2. Blood pressure …………………………… Hemoglobin ………………………
3. Hearing ……………………………………………………
4. Urine (a) Albumen………………………… (b) ............................
5. a) Venereal diseases…………………(b) Bilharzia............................

6. Pregnancy …………………………………………………………
7. Neurosis……………………………………………………………
8. Is there any abnormality of :(a) The heart…………………………….

   b) Lungs ……………………… c) The spleen …………………

9. Are there serious diseases. E.g. Leprosy, Epilepsy, Asthma, Diabetes, etc. ……………………………………………………………………………...

Date ……………… Signature of the medical Officer ……………… Station …………………

Designation ……………………

**FOMU NAMBA 2.**

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI.**

1. (a) Jina la mwanafunzi …………………………………………………...

   (b) Anuani …………………………………...

2. Tarehe ya kuzaliwa ……………………………………...
3. Shule aliyomalizia darasa la saba ………………………… Mwaka ……………………………………………….
4. Mkoa anaotoka ………………………… Wilaya alipozaliwa ……………………………...
5. Tarafa anayotoka ………………………... Kata atokayo ……………………
6. Kijiji anachotoka …………………………... Mtaa anaotoka ………………
7. Jina la Mtendaji wa (a) Kata ………………………. (b) Mtaa/Kijiji ………
8. Jina la (a) Balozi wa nyumba kumi ……………………….

   (b) Mwenyekiti wa Mtaa ……………………………

9. Michezo anayopendelea

| **Na.** | **Jina la Mchezo** |
|---|---|
| 1. | |
| 2. | |
| 3. | |

11. Nafasi yoyote ya uongozi aliyowahi kushika

| **Na.** | **Aina ya Uongozi** | **Shule** | **Mwaka** |
|---|---|---|---|
| 1. | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2. | | | |
| 3. | | | |

Nathibitisha kwamba taarifa nilizozitoa hapo juu ni za kweli, pia nathibitisha kuwa nitakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi pamoja na kuwa na bidii ya masomo na sitapata chini ya alama 50 kati ya 100 kwa kila mtihani, zoezi au jaribio nitakalofanya hapa shuleni.

**Jina la Mwanafunzi …………………………………….. Sahihi ………………. Tarehe ………….**

## FOMU NAMBA 3.

### TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI

1. Jina kamili la Mzazi/Mlezi ………………………………………………….
2. Kazi anayofanya mzazi …………………………………………………
3. Anuani ……………………………………………………….
4. Namba ya simu …………………………………….
5. Mkoa ……………………. Wilaya ……………… Tarafa ………………… Kata ……………………………… Kijiji ……………………. Mtaa ……………

6. Anuani kamili ya nyumbani ambako mwanafunzi atakuwa anakwenda wakati wa likizo

   Mahali ……………………………………. kwa nani ……………………

7. Majina ya viongozi/Wazazi /walezi atakakokuwa anakwenda wakati wa likizo
   - Jina la Baba /mlezi/ndugu ……………………………………...
   - Jina la mama/mlezi ……………………………………………………
   - Mtendaji wa Kata ………………………………………….…
   - Mtendaji wa Kijiji/Mtaa ……………………………………..……
   - Mwenyekiti wa Kijiji/Mtaa ……………………………………………

### TAMKO LA MZAZI

Mimi Mzazi/Mlezi wa..........................................................................................ninaahidi

kushirikiana na walimu pamoja na watumishi wote wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Liuguru katika kumlea mwanangu kwa muda wote atakapokuwa shuleni.

Nitaomba kujulishwa mara moja endapo mwanangu ameenda kinyume na sheria, kanuni na taratibu za shule. Pia nitakuwa tayari mwanangu kupewa adhabu inayostahili kwa makosa atakayofanya. Ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule pale itakapobidi.

**Jina la Mzazi/Mlezi ………………. Sahihi ……....…… Tarehe ……………**

**FOMU NA.4**

**<u>FOMU MAALUM YA TAARIFA ZA NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI</u>**

Ndugu wa karibu wa mwanafunzi: Hakikisha unaandika majina matatu na anwani zao.

Hii inasaidia shule kutoa taarifa endapo tatizo litatokea.

**(Ambatanisha passport size 4 za ndugu wa karibu)**

**1. (a)Jina ________________**

(b) Uhusiano: ____________________________________

(c) Anwani:_______________________________________________________

(d)Namba ya Simu:_____________________________________________ Saini ya mzazi/Mlezi: __________________________________

Tarehe: ____________________________________

**2 .(a)Jina_____________________________________________________________**

(b) Uhusiano: __________________________________________________

(c) Anwani:____________________________________________________

(d) Namba ya Simu:_____________________________________________

Saini ya mzazi/Mlezi: ______________________________

Tarehe: ____________________________________

**3. (a)Jina_____________________________________________________________**

(b) Uhusiano: _____________________________________

(c) Anwani:____________________________________________________

(d) Namba ya Simu:____________________________________________

Saini ya mzazi/Mlezi: ______________________________ Tarehe: _

**4. (a)Jina**_______________________________________________

(b) Uhusiano: _____________________________

(c) Anwani:_________________________________________

(d) Namba ya Simu:__________________________________

Saini ya mzazi/Mlezi: _______________________

Tarehe: ____________________________

**FOMU NAMBA 5 MKATABA/TAMKO LA MWANAFUNZI**

Mimi……………………………………………………………………...……

(jina kamili) ambaye ni mwanafunzi, nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa, ninakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na shule hii. Ninaelewa wazi kwamba shuleni ni mahali pa kujifunza na mimi nina nia ya kujifunza. Ninaelewa pia kuwa nafasi hii niliyopewa ni dhamana, hivyo naahidi mbele ya wazazi/walezi wangu ya kwamba nitaitumia vema nafasi hii kwa kushirikiana na uongozi wa shule kutimiza na kutekeleza yale yote yaliyoelekezwa katika fomu hii. Nitatii na kufuata sheria zote za shule wakati wote. Naahidi kutoshiriki katika mgomo, fujo, makosa ya jinai na makosa mengine yaliyotajwa. Naahidi pia kufanya bidii katika masomo yangu na kuhakikisha ninapata ufaulu wa Alama za juu hususani katika masomo ya Sayansi na kuendelea na Kidato cha Tano. Aidha, naahidi kuwa na ushirikiano mzuri na wanafunzi wenzangu na kuwa mfano bora wa Taasisi ya Shule ya Sekondari ya Wasichana Liuguru (Liuguru Girls) ndani na nje ya shule.

**Saini ya mwanafunzi** ………………………………………………………

**Tarehe**………………………………………